HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA UTAMBULISHO WA MKANDARASI NA MHANDISI MSHAURI WA MRADI WA TACTIC (TANZANIA CITIES TRANSFORMING INFRASTRUCTURES COMPETITIVENES) KWA WADAU WA MAENDELEO MKOANI RUKWA TAREHE 23 OKTOBA, 2023

- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu,***
- ***Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Sumbawanga,***
- ***Katibu wa CCM Wilaya ya Sumbawanga,***
- ***Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,***
- ***Katibu Tawala Wilaya ya Sumbawanga,***
- ***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga,***
- ***Wahe. Madiwani,***
- ***Wakuu wa Idara na Vitengo Manispaa ya Sumbawanga,***
- ***Mkandarasi wa Mradi wa TACTIC,***
- ***Mhandisi Mshauri wa Mradi wa TACTIC,***
- ***Watumishi wa Halmashauri,***
- ***Wadau Mbalimbali wa Maendeleo,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Mabibi na Mabwana,***

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye Afya njema. Kipekee niwashukuru sana uongozi

wa Manispaa ya Sumbawanga kwa kunialika kuhudhuria tukio hili la utambulisho wa mkandarasi na mhandisi mshauri wa mradi wa TACTIC (Tanzania Cities Transforming Infrastructures Competitivenes).

Ndugu Washiriki, Mkoa wa Rukwa kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilipata bahati ya kuingizwa kwenye mpango wa kutekeleza miradi ya Uimarishaji Miji Tanzania; TSCP, DMDP zilizotekelezwa kwa Halmashauri za Majiji na ULGSP (Urban Local Government Strengthening Programme), iliyotekelezwa katika jumla ya Halmashauri 18 za Manispaa na Miji Tanzania Bara kuanzia mwaka 2013 hadi Desemba, 2020. Miradi hiyo ilionekana kutekelzwa kwa ufanisi na kuleta tija kwa Halmashauri zilizobahatika kuipata katika kuimarisha; Miundombinu ya Barabara, Masoko, Stendi za mabasi na malori, machinjio, mifumo ya uhifadhi taka ngumu na taka miminika, kuimarisha mifumo ya Ukusanyaji Mapato, Matumizi ya TEHAMA, kuwezesha uandaaji wa Mipango Kabambe katika miji na matumizi ya Ardhi pamoja na kuwezesha mafunzo mbalimbali (Capacity Building) kwa wafanyakazi wa sekta mbalimbali na kuongeza vifaa vya ofisi katika kuboresha ufanisi.

Ndugu Washiriki, Katika kutekeleza mpango wa ULGSP, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilifanikiwa kutekeleza miradi ya Ujenzi wa barabara za lami (Asphalt concrete) kilometa 11.7 katika Kata 6 za mjini (Mazwi, Katandala, Izia, Majengo, Msua na Chanji), Ujenzi wa Stendi ya Mabasi iliyoko Katumba Azimio, Kata ya Pito, Ujenzi wa Kituo cha Kuegesha magari Makubwa kilichoko Utengule Kata ya Lwiche, Ununuzi wa gari moja na ghuba 44 za kukusanya na kusomba taka ngumu, Kuandaa Mpango Kabambe wa Mji (General Planning Scheme - GPS), Kuimarisha Mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri, Ununuzi wa vifaa vya Ofisi na Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri.

Ndugu Washiriki, Kutokana na ufanisi wa miradi hiyo, ilionekana muda wa utekelezaji umekuwa mfupi kulinganisha na mahitaji kwa kipindi kilichowekwa. Hivyo, serikali ikaona hitaji la kuongeza muda wa kutekeleza miradi mingi zaidi, ikaja na wazo la kuendelea kuzisaidia Halmashauri zake katika kuteleza miradi iliyosalia kwa njia ya program nyingine kama huu wa TACTIC ambao ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji unaofadhiliwa na Serikali Kuu kwa Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Programu ya TACTIC-(Tanzania Cities Transforming Infrastructures Competitivenes), inatarajia kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, 2022/2023 hadi 2027/2028 katika Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji. Utekelezaji wake umegawanywa katika awamu tatu, na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga imepata bahati ya kuingizwa kwenye Halmashsuri 12 za awamu ya kwanza baada ya kufanya vizuri katika awamu ya ULGSP. Hivyo, kupewa jukumu la kuainisha miradi kulingana na vipaumbele.

Ndugu Washiriki, Katika awamu hii ya kwanza ya Miradi ya TACTIC Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga itatekeleza Miradi ya Ujenzi wa soko la mazao Kanondo ambapo patajengwa Vyumba/Vizimba 400 vya biashara, Maghala ya kuhifaa mazao, Kufunga vifaa vya kusafisha, kuchambua na kuhifadhi kwenye mifuko kwa vipimo vilivyokubalika na Kujenga vyumba vya taasisisi za fedha katika eneo la Kanondo. Mradi mwingine ni Ujenzi wa Barabara za lami (Kiwango cha Asphlt) jumla ya Kilometa 14.2 (Barabara ya Maweni II Km 0.4, Sokolo-Bible-Mbeya Rd Km 2.6, Kalangasa Rd Km 0.5, Kasema Rd Km 0.4, Maendeleo Rd Km 0.2, Muva Rd Km 0.2, Kimati - Ufipa Rd Km 0.2, Airport - Senga - Wipanga Rd Km 3.0, Sido – Senga - Mafulala Rd Km 2.7, Kuzunguka Hospitali ya Wilaya Isofu –Km 2.0, na Kuzunguka Soko la mazao Kanondo –Km 2. Barabara hizi zikikamilika zitapunguza sana kero kwa Wananchi wetu,

Aidha Soko la Mazao litakalojengwa eneo la Kanondo litakuwa Msaada sana kwa Wakulima wetu ambao watauzia mazao yao eneo moja badala ya kulanguliwa huko mitaani kwa bei ya chini ambayo wakati mwingine sio hata ya Soko. Niwatake wasimamizi wote wa Miradi hii pamoja na Wakandarasi kuhakikisha kuwa Miradi inakamilika kwa muda uliopangwa kwenye mikataba na kwa ubora. Visingizio vyovyote vya kutokamilisha miradi hii kwa wakati mimi pamoja na Wananchi wenzangu wa Mkoa wa Rukwa hatutovielewa.

Ndugu Washiriki, Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa natoa Shukrani nyingi sana kwa Serikali yetu ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kutupatia fulsa nyingine ya kutekeleza miradi ya kuimarisha mji wetu. Aidha, kukamilika kwa miradi hii kutaiwezesha Halmashauri yetu kupendeza, Kuongeza mapato kupitia tozo kwa miundombinu iliyojengwa na kuinua uchumi wa wananchi kwa kuokoa muda wa kusafiri kutoka eneo moja hadi jingine.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,
Asanteni kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere
MKUU WA MKOA WA RUKWA